

Miongozo ya Huduma na Shughuli kwa Vijana.

Kanuni na miongozo hii imekusudiwa kuwasaidia viongozi wa vijana na watu wazima pale wanaposhauriana pamoja katika kupanga fursa za huduma zenye maana na shughuli nzuri, za kufurahisha. Kanuni na miongozo hii pia inaweza kutumika kama nyenzo katika mikutano ya kigingi, kata, na mikutano ya baraza la vijana.

KANUNI

Shughuli zinapaswa kupangwa na kufanywa na viongozi wa akidi na madarasa, kwa msaada kutoka kwa washauri ambao ni watu wazima. Shughuli zinapaswa:

- Kuimarisha imani ya kizazi kinachoinukia kwa Baba wa Mbinguni na Mwanawe, Yesu Kristo, na kuwasaidia vijana na familia zao kuendelea katika njia ya agano wanapokumbana na changamoto za maisha.
- Kuwasaidia vijana kukamilisha kazi ya wokovu na kuinuliwa (ona *General Handbook: Serving in The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints* [2020], 1.2, [ChurchofJesusChrist.org](https://www.churchofjesuschrist.org)).
- Kuwapa vijana msaada na kuwafanya wahisi kuwa sehemu ya, kwa kuimarisha umoja wa darasa na akidi na kwa kujenga mahusiano yao na makundi rika, viongozi, na familia.
- Kutoa fursa zenye usawa kwa vijana kuwatumikia wengine na kukua kiroho, kijamii, kimwili na kiakili (ona [Luka 2:52](#)).
- Kutoa uzoefu ambao unawasaidia wavulana na wasichana kuijandaa kutimiza majukumu yao matakatifu.
- Kufuata usalama wote wa Kanisa na sera na miongozo mingine (ona [Safety.ChurchofJesusChrist.org](#)).

MIONGOZO

Miongozo ifuatayo inaweza kutoholewa kuendana na hali ya eneo, chini ya maelekezo ya viongozi wa eneo:

- Fanya huduma na shughuli kila wiki pale inapowezekana. Huduma na shughuli zinaweza kufanywa mara chache kulingana na mahitaji na hali za washiriki wa akidi na darasa lakini zinapaswa kufanyika angalau kila mwezi.
- Tengeneza kalenda ya angalau miezi mitatu ijayo. Hii itahakikisha kwamba usawa wa shughuli mbalimbali zenye malengo na changamoto, kwa kuzingatia kanuni zilizo hapo juu, zinapangwa kukidhi mahitaji ya washiriki binafsi wa akidi na darasa.
- Tafuta fursa kwa ajili ya vijana kutoa huduma zenye maana kwa watu binafsi, familia, na jamii. Fikiria mahitaji na mapendeleo ya kila mshiriki wa akidi na darasa wakati ukiwahimiza kutojiangalia zaidi wao wenyewe.
- Kwa sababu shughuli za pamoja za wavulana na wasichana zina faida hasa, zifanye kila mwezi pale inapowezekana. Shughuli za pamoja za vijana wakubwa zinaweza kufanywa mara nyingi zaidi.
- Wape vijana fursa za kuhudhuria mikutano na kambi:
 - Vijana wanaofikia umri wa miaka 14 na zaidi watahudhuria mkutano mmoja wa Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana kila baada ya mwaka mmoja. Mikutano na matembezi ya vijana vinaweza kufanyika kwa miaka kadhaa wakati ambapo mkutano wa Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana haufanyiki.
 - Kambi za Wasichana na kambi za akidi ya Ukuhani wa Haruni zinaweza kufanyika kila mwaka.
 - Kambi za ziada za usiku kucha na shughuli vinaweza pia kufanyika. Kwa ajili ya wavulana, kambi tatu hadi sita za usiku kucha au shughuli za kila mwaka zinahimizwa, pale inapowezekana.
- Pata mawazo kwa ajili ya shughuli za akidi na darasa kwenye [ChurchofJesusChrist.org/youth/activities](https://www.churchofjesuschrist.org/youth/activities). Tumia [Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana \(2011\)](#) kama nyenzo katika kupanga shughuli.

NYENZO

- *General Handbook*, sura 10, 11, na 20
- [YoungWomen.ChurchofJesusChrist.org](https://www.youngwomen.churchofjesuschrist.org)
- [AaronicPriesthoodQuorums.ChurchofJesusChrist.org](https://www.aaronicpriesthoodquorums.churchofjesuschrist.org)